

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)

**SHERIA NDOGO ZA (ADA YA VIBALI VYA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA
MANISPAA YA TABORA, 2014**

Jina na tarehe ya kuanza kutumika 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada ya vibali vya Ujenzi) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za Mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoeleza vinginevyo; -

“Afisa Muidhiniwa”maana yake ni Afisa yejote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

“Halmashauri”maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Tabora

“Kibali” maana yake ni ruhusa au idhini itakayotolewa na Halmashauri kuruhusu ujenzi wa jengo lolote katika maeneo maalum

“Jengo” maana yake ni nyumba iwe imekamilika kujengwa au iliyojengwa kwa mawe, matofali ya kuchoma, matofali ya sementi na ambayo imeezekwa kwa bati, vigae au asbestos.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja

na Afisa ye yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

Maombi ya kibali 4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetaka kujenga jengo la aina yoyote katika maeneo maalum kuomba na kupata kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri.

(2) Maombi ya kibali cha ujenzi yataambatanishwa pamoja na ramani ya jengo iliyochorwa na mtaalam anayetambuliwa kisheria;

Masharti ya kibali 5.-(1) Halmashauri haitatoa kibali hadi mwombaji awe ametimiza mambo yafuatayo;:-

- (a) amewasilisha michoro ya ramani ya jingo;
- (b) amelipa ada ya ukaguzi wa ramani .
- (c) awe na kiwanja au eneo linalotambulika ambalo anatakiwa kujenga jengo hilo.

(2) Ramani zitakazowasilishwa zitatakiwa kuwa na vipimo vitakavyokubaliwa na Afisa Muidhinishwa.

(3) Baada ya mwombaji kutimiza masharti yaliyotajwa katika kifungu cha 5(1) na baada ya ramani kukaguliwa na kupidishwa na Afisa Ardhi, Mhandisi wa Ujenzi, na Afisa Mipango Miji, Halmashauri itatoa kibali cha ujenzi.

Muda wa kuanza ujenzi 6.-(1) Mwombaji atatakiwa kuanza ujenzi katika muda wa siku tisini (90) kuanzia tarehe ya kupewa kibali.

(2) Mtu ye yeyote atakayeanza shughuli za ujenzi bila kuwa na kibali atakuwa ametenda kosa.

Uwezo wa Afisa Muidhini-wa 7-(1) Afisa Muidhiniwa anaweza wakati wowote wa kazi kuingia katika eneo lolote ambalo ujenzi unafanyika kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi.

(2) Endapo Afisa Muidhiniwa atabaini kuwa mjenzi hana kibali au Mjenzi anajenga jengo hilo kinyume na masharti ya kibali na kinyume cha ramani iliyoidhinishwa na Halmashauri, Halmashauri itatoa notisi ya kusimamisha ujenzi, au kubomoa jengo hilo katika muda utakaooneshwa katika Notisi hiyo.

Halmashauri 8.-(1) Halmashauri inaweza kukataa kupidisha ramani endapo:-

- kutoidhini-sha ramani (a) ujenzi unaokusudiwa kufanywa unavunja Sheria, Kanuni na Taratibu za ujenzi;
- (b) ramani zilizowasilishwa hazikidhi masharti ya ujenzi;
- (c) itabainika kuwa mwombaji sio mmiliki halali wa kiwanja au eneo ambalo jengo linakusudiwa kujengwa
- (2) Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi ujenzi wa majengo ya Serikali hautahitaji kuwa na kibali.
- Adhabu (3) Mtu ye yote atakayevunja au kushindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja faini na kifungo.
- Kufifilisha kosa 7. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtaka mtu aliyekiri kufanya kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kulipia kiasi cha fedha kisichozidi kiwango cha juu cha faini kilichowekwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI

Chini ya kifungu cha 4(3)

ADA YA KIBALI CHA UJENZI

MAJENGO YA MAKAZI

1.	Eneo la sakafu isiyozidi mita za mraba 50	Ada ya kibali Tshs 10,000/=
2.	Eneo la sakafu inayozidi mita za mraba 50 lakini isiyozidi mita 100	Ada ya kibali Tshs 15,000/=
3.	Eneo la sakafu inayozidi mita 100 lakini haizidi mita za mraba 200	Ada ya kibali Tshs 20,000
4.	Eneo la sakafu inayozidi mita 600 za 600 laini haizidi mita za mraba 900	Ada ya kibali Tshs 100,000/=

MAJENGO YA BIASHARA

Ada ya kibali=mita za mraba *Tshs 500/=

MAJENGO YA VIWANDA

Ada ya kibali=mita za mraba*Tshs 600/=

MAJENGO YA GHOROFA

Ada ya kibali=mita za mraba*Tshs 600/=

MAJENGO YA MAGHALA

Ada ya kibali=mita za mraba*Tshs 600/=

UZIO WA KUTA

(i)MAENEKO YA KUISHI

Ada ya kibali jumla ya urefu*Tshs 500/=

(ii)MAENEKO YA BIASHARA

Ada ya kibali=jumla ya urefu*Tshs 1,000/=